

NAFASI YA JAZANDA KATIKA UWASILISHAJI WA MAUDHUI YA MAPENZI NA MAUMIVU YA KIHISIA: MIFANO KUTOKA WIMBO WA *KIZA KINENE*

Shadidu A. Ndossa

Chuo Kikuu cha St John cha Tanzania

ashadidu@sjut.ac.tz

Ikisiri

Makala hii inajadili matumizi ya jazanda katika wimbo wa Kiza Kinene wa msanii maarufu wa muziki wa kizazi kipyua kutoka Tanzania, Nandy, kwa kushirikiana na kundi la muziki la Sauti Sol kutoka Kenya. Kwa kutumia Nadharia ya Uihakiki wa Fasihi Jamii, makala inatathmini jinsi jazanda zinavyotumika kama mbinu ya kisanaa katika kuakisi mazingira halisi ya kijamii, kihisia na kiutamaduni ya wasanii na jamii zao. Aidha, makala inaonesha kuwa jazanda zilizopo katika wimbo huu zinahusiana na viungo vya mwili, mazingira ya asili, familia, biashara na imani za jadi, zikielezea kwa kina hisia za maumivu, upweke, usaliti na matarajio yaliyofifia katika mapenzi. Makala inahitimisha kuwa jazanda si mapambo ya lugha pekee bali ni nyenzo muhimu ya mawasiliano yenye mguso wa kijamii, kiitikadi na kihisia, inayomwezesha msanii kuwasilisha ujumbe mzito kwa namna ya ubunifu na isiyo ya moja kwa moja.

Dhana za Msingi: Jazanda, Maana Fiche, Muziki, Sanaa

1.0 Utangulizi

Sanaa ya muziki imeendelea kuwa chombo muhimu cha mawasiliano ya kijamii, kisiasa, kihisia na kitamaduni. Wasanii hutumia lugha ya picha na mbinu mbalimbali za kifani ili kufikisha ujumbe wao kwa hadhira kwa njia yenye mvuto na mguso wa kihisia. Mojawapo ya mbinu hizo ni jazanda—ambayo katika muktadha wa makala hii inarejelea taswira au usemi unaobeba maana fiche, ya ndani au ya kupindisha, ambayo huibua tafsiri pana zaidi ya hali, tukio au hisia

fulani, tofauti na maana yake ya moja kwa moja. Jazanda huweza kuwa maneno, taswira au miundo ya lugha inayomfanya msikilizaji atafakari zaidi ili kuuelewa ujumbe unaofichwa.

Jazanda hutoa nafasi kwa wasanii kujieleza kwa ubunifu na huwahusisha wasikilizaji katika kutafsiri ujumbe kwa undani zaidi. Msanii Faustina Charles Mfinanga, anayefahamika kwa jina la kisanii kama Nandy, ni miongoni mwa wanamuziki wa Kiswahili waliobobea katika matumizi ya jazanda. Kupitia nyimbo zake maarufu kama *Kivuruge*, *Ninogeshe*, *Nikumbushe*, *Nimekuzoea* na *Kiza Kinene*, Nandy huwasilisha masuala ya mapenzi, machungu ya usaliti, matumaini, na matatizo ya kijamii kwa kutumia lugha ya picha iliyojaa jazanda.

Katika wimbo wa *Kiza Kinene*, Nandy ameshirikiana na Sauti Sol, kundi maarufu la muziki kutoka Kenya linalojulikana kwa umahiri wake wa kuoanisha midundo ya *Afro-pop*, *Sol* na *R&B* na tungo zenye kina cha kijamii na kihisia. Sauti Sol wamekuwa na mchango mkubwa katika muziki wa Afrika Mashariki na kimataifa, na wana sifa ya kutumia sauti zao zenye mchanganyiko wa utulivu, hisia na uhalisia wa maisha ya Kiafrika.

Makala hii inalenga kuelezea aina za jazanda zinazotumika katika wimbo wa Nandy na Sauti Sol, maana zinazojengwa na jazanda hizo, nafasi ya jazanda katika kubeba na kuwasilisha ujumbe wa msanii, na mwisho kuelezea sababu zinazowafanya wasanii hawa waitegemee jazanda kama mbinu ya kisanaa. Kwa kufanya haya yote, makala hii inachangia uelewa mpana wa matumizi ya lugha ya picha katika muziki wa Kiswahili na umuhimu wa mbinu za kifani katika kuboresha usambazaji wa ujumbe kwa hadhira.

2.0 Maelezo Mafupi kuhusu Wimbo Teule

Wimbo unaochambuliwa katika makala hii ni kazi ya ubunifu iliyoandikwa na kutungwa kwa ushirikiano kati ya msanii nyota kutoka Tanzania, Nandy, na kundi mashuhuri kutoka Kenya, Sauti Sol. Wimbo huu ulitoka takriban miaka mitano iliyopita. Tangu wakati huo umekuwa maarufu sana katika nchi za Afrika Mashariki na hata nje ya bara la Afrika.

Wimbo wa *Kiza Kinene* unaangazia maudhui ya mapenzi yenye changamoto, ukilenga zaidi hali ya sintofahamu, huzuni, maumivu, na kukosa mwelekeo katika uhusiano wa kimapenzi. Mashairi

ya wimbo huu yamejaa jazanda mbalimbali zinazobeba maana fiche, taswira za kijamii na hali halisi ya maisha ya watu wa kawaida. Wasanii wanazungumzia mapenzi yaliyofifia, kukatishwa tamaa, na hisia za upweke huku wakitumia lugha ya picha kuelezea masaibu hayo.

Kwa kutumia mazingira ya nyumbani, biashara, teknolojia duni, na hata imani za jadi kama vichocheo vya kueleza maumivu ya kimapenzi, wimbo huu umefanikiwa kuunganisha sanaa na maisha halisi ya watu wa tabaka tofauti. Hali hii imeufanya wimbo huu kukubalika na kupigwa katika redio na televisheni mbalimbali nchini Kenya, Tanzania, na maeneo mengine ya dunia. Aidha, video ya wimbo huu imepokelewa vizuri katika majukwaa ya kidijiti kama *YouTube*, ikivutia watazamaji zaidi ya milioni nane hadi kufikia mwezi wa sita wa mwaka 2025.

Kwa ujumla, wimbo huu siyo tu kazi ya burudani, bali ni kioo cha maisha halisi ya mapenzi, changamoto zake, na namna watu wanavyojaribu kuyatafsiri kwa kutumia mazingira yanayowazunguka. Ushirikiano kati ya Nandy na Sauti Sol umeongeza mvuto na utofauti wa kisanaa, na hivyo kuufanya wimbo huu kuwa na uzito wa kijamii, kisanaa, na kihisia.

3.0 Nadharia Iliyotumika

Katika uchambuzi wa makala hii, imetumika *Nadharia ya Uhakiki wa Fasihi Jamii* ambayo huzingatia uhusiano kati ya kazi ya fasihi na mazingira ya kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na kiitikadi. Nadharia hii huchukulia fasihi kuwa zao la jamii na kioo kinachoakisi maisha ya watu waliomo katika jamii hiyo. Miongoni mwa waanzilishi na wachangiaji wakuu wa mtazamo huu ni Georg Lukács (1962) na Raymond Williams (1977) ambao walisisitiza kuwa kazi ya fasihi huundwa kwa kuzingatia hali halisi za kijamii, tabaka, na historia ya jamii.

Katika muktadha wa Kiafrika, Ngũgĩ (1986) ameendeleza wazo hili kwa kueleza kuwa fasihi haiwezi kutenganishwa na jamii kwani ni sehemu ya mapambano ya kijamii, kitamaduni na kiitikadi. Nadharia hii huamini kuwa kazi ya fasihi hutokana na jamii na kwa ajili ya jamii, na kwamba maudhui ya kazi ya fasihi hujengwa juu ya uzoefu wa maisha ya watu na hutumika pia kuibua mijadala na kuchochea mabadiliko ya kijamii. Kwa muktadha wa makala hii, nadharia hii imesaidia kuelewa kwa kina namna jazanda zinazotumiwa na wasanii Nandy na Sauti Sol zinavyoakisi maisha halisi ya jamii yao kwa kuanzia mahusiano ya kimapenzi, maumivu ya

usaliti, matumaini, mpaka misingi ya kitamaduni na kihisia. Jazanda hizo si mapambo ya lugha tu bali ni mbinu za kifasihi zinazosaidia kufikisha ujumbe wa kijamii, jambo linalothibitisha kuwa muziki wao ni sehemu hai ya fasihi simulizi ya kisasa inayobeba taswira za maisha ya jamii yao.

4.0 Dhana ya Jazanda

Kwa mujibu wa Okwena (2017), jazanda ni mbinu ya fasihi inayotegemea taswira, inayotumia ulinganishi wa moja kwa moja bila viunganishi. Kwa maneno mengine, inafanya kazi ya kulinganisha vitu viwili bila kutumia “kama” au “ni,” ili kuleta picha zinazoonekana akilini na kuipa maana ya kina zaidi na ya msingi. Wasanii na waandishi hutumia jazanda—yaani kulinganisha moja kwa moja bila kutumia viunganishi kama "kama" au "ni" kufikisha hisia zao kuhusu vitu au hali mbalimbali. Hali hizi zinaweza kuhusu furaha, matumaini au hata maumivu. Hivyo basi, tunaweza kusema kwamba jazanda ni mbinu ya kisanaa yenye lengo la kuunda taswira au picha za akilini mwa msomaji au msikilizaji na hutumika kuelezea mambo mazito kwa njia ya mficho. Kwa mfano, msomaji au msikilizaji wa kazi ya fasihi anaposikia “*Wewe ni asali yangu ya moyo*”, ujumbe unaopatikana hapa ni kuwa mpenzi wake ana ladha ya utamu. Vilevile, msikilizaji anaposikia “*Wewe ni nuru ya macho yangu*” inaonyesha wazi namna mhusika anavyomwona mpenzi wake kama mwangaza na mwelekeo mzuri wa mapenzi yao.

Kwa upande mwingine, jazanda zinazorejsha maumivu zinaweza kuwa kali kama “*Wewe ni giza maishani mwangu*” au “*Wewe ni kaburi/kizingiti katika maisha yangu*”, mifano yote miwili inaonesha hisia nzito, huzuni au kipigo cha kimwili au kisaikolojia. Jazanda hizi ni za karibu sana—zinatangazwa bila kificho, moja kwa moja kama njia ya kuingiza msomaji au msikilizaji ndani ya hali ya kihisia ya mhusika. Kwa njia hii, jazanda hutoa picha zinazoonekana akilini, zikichangia kuongezea maana na ubunifu katika kazi ya fasihi. Kupitia ulinganishaji huu, msomaji anaweza kuhisi furaha au maumivu ya mhusika moja kwa moja, na ujumbe unafika kwa undani na uhalisia zaidi. Katika sehemu inayofuata makala imeelezea aina mbalimbali za jazanda zilizotumika katika wimbo teule na namna zinavyowakilisha maumivu ya kimapenzi kwa wasanii. Jazanda hizo ni zile za kimazingira, imani za jadi, nyumbani na biashara. Kwa kuanza

mwandishi anafafanua kuhusu matumizi ya jazanda za viungo vya mwili na na jinsi ilivyotumika kuwakilisha maumivu ya kimapenzi.

4.1 Jazanda za Viungo vya Mwili

Katika ujenzi wa maana na uwasilishaji wa hisia fiche, mtunzi wa wimbo *Kiza Kinene* ametumia kwa ustadi jazanda zinazohusisha viungo vya mwili ili kuonyesha hali ya ndani ya kihisia, hasa maumivu na mkanganyiko wa kimapenzi. Miongoni mwa jazanda hizi ni “macho” na “mboni” ambayo yanaibuka kama ishara ya hali ngumu ya mapenzi yasiyo na mwelekeo wala matumaini.

Katika mstari wa Nandy, “Haioni mboni yangu / macho,” mpenzi anaelezwa kuwa hawezi tena kuona mboni au macho ya mpenzi wake, hali inayoweza kutafsiriwa kuwa ni upofu wa kimapenzi au kutokuwapo tena kwa mawasiliano ya kihisia kati ya wahusika. Macho, katika muktadha huu, siyo tu kiungo cha kuona, bali ni kielelezo cha kuelewana, kuelewa hisia, au kuonesha mapenzi. Kukosekana kwa “mtazamo” huu ni sawa na kupotea kwa kiunganishi muhimu cha mapenzi kati ya wapenzi hao.

Hii ni jazanda ya kimajazi inayotumia kiungo cha mwili kuashiria hali ya ndani ya kihisia. Kupitia macho na mboni, msanii anaonyesha hali ya kutokueleweka, kutoonekana au kupuuzwa katika mahusiano. Hii ni hali ya kupoteza matumaini, ambapo mtu anajiona hayupo tena katika “rada” ya mpenzi wake. Jazanda hii ni mwafaka kabisa katika kujenga picha ya mgogoro wa kimapenzi usioeleweka kwa urahisi. Inatoa nafasi ya kuona kwa ndani ya mhusika ambayo haionekani kwa nje bali inasikika kupitia sauti ya mshairi/msanii.

Maelezo ya wasanii hawa yanaungwa mkono na Ibrahim (2022) ambaye anaona kuwa msanii anaweza kuelezea hisia za ndani na fiche kwa kutumia lugha ya picha, mwitikio wa kihisia na jazanda zenye kuibua taswira ya mguso wa nafsi. Kauli hii inathibitisha kuwa matumizi ya viungo vya mwili kama jazanda ni mbinu ya kifasihi inayotumika kwa mafanikio kueleza mateso ya kimapenzi ambayo hayawezi kusemwa kwa maneno ya moja kwa moja.

4.2 Jazanda za Kimazingira

Katika ujenzi wa hisia za mateso ya kimapenzi, wasanii wametumia jazanda zinazotokana na mazingira ya asili kuibua picha nzito za kukata tamaa na kuporomoka kwa matumaini. Mifano kama vile “kiza kinene,” “(nipo) juu ya mawe,” na “katibua maji kisimani” ni vielelezo vya matumizi ya mandhari ya mazingira kuwasilisha hali ya hisia zilizokithiri. Hizi ni jazanda zenye mizizi katika mazingira ya kawaida lakini zinageuzwa kuwa alama za mateso ya ndani.

Kauli ya “kiza kinene” hutoa taswira ya giza lisilo na mwanga wala matumaini. Giza hili siyo la kimwili pekee, bali ni fumbo la mkanganyiko wa kihisia, kutokuwa na dira au mwelekeo katika mapenzi. Katika muktadha huu, mazingira yanageuka kuwa kiwakilishi cha hali ya ndani ya nafsi ya wahusika. Vivyo hivyo, kusema “roho ipo juu ya mawe” ni taswira ya kuachwa katika hali ngumu, isiyo na faraja ambapo mawe yanawakilisha ugumu na kutojali wa mazingira yanayowazunguka wahusika (Okwena, 2013)

Mfano mwingine ni “katibua maji kisimani,” ambapo wasanii wanatoa picha ya kuchafua au kuharibu chanzo cha matumaini au upendo. Kisima, kama alama ya maisha au matumaini, kikishatibuliwa, kinapoteza thamani na uhai wake. Hii ni jazanda yenye uzito wa kihisia na uhalisia wa kimazingira. Kama anavyodokeza Buell (1995), fasihi ya mazingira huwa na uwezo wa kutumia mazingira kama kioo cha nafsi ya binadamu na kueleza migogoro ya ndani kwa kutumia taswira za kimazingira. Buell (ameshatajwa) anaeleza kuwa utamaduni wa mazingira una nafasi ya “kutoa sauti kwa mazingira yaliyonyamazishwa,” jambo ambalo linaonekana wazi hapa—ambapo mazingira si tu mandhari bali wahusika wenyewe wa kihisia.

Vivyo hivyo, Manes (1996) anasema kwamba mazingira mara nyingi huoneshwa kuwa kimya, lakini kimya hicho kinaweza kuwa chenye maana kubwa, hasa katika fasihi. Ukimya wa mazingira kama “mawe,” “kiza,” au “kisima kilichochafuka” si wa kutoweza kusema, bali ni ukimya wenye sauti ya huzuni na onyo.

Kwa ujumla, matumizi ya jazanda za kimazingira katika wimbo huu yanatilia mkazo hali ya kupoteza matumaini na uharibifu wa ndani ya nafsi kupitia lugha ya picha zinazotokana na mazingira. Wasanii wametumia mazingira si tu kama mandhari bali kama njia ya kuongeza uzito

wa hisia na kueleza yaliyoshindikana kusemwa moja kwa moja. Kama Okwena (2017) anavyosema kuwa matumizi ya jazanda za kimazingira ni njia mwafaka kwa kuwa yale yanayosemwa yanafahamika vema kwa wanaoambiwa kwa kuwa yanasadifu mazingira yao halisi.

4.3 Jazanda za Nyumbani

Wasanii Nandy na Sauti Sol wanatumia jazanda za nyumbani si tu kuonesha mandhari ya karibu na ya kila siku, bali pia kuibua hisia za ndani zilizojificha nyuma ya picha za vitu vya kawaida. Kwa kutumia vitu vya kawaida vinavyotumika katika maisha kama kitanda, shati na chumba wasanii wanaunda mazingira yanayoakisi hali ya mtu anapojikuta katika uhusiano unaomsumbua kisaikolojia na kihisia. Kwa mfano, katika ubeti wa pili, Sauti Sol wanasema "Chumbani kwangu kaingia kunguni gani, mara kwenye kitanda mara kwa shati". Katika nukuu hii, kunguni si mdudu wa kawaida wa majumbani tu, bali ametumika kama jazanda inayowakilisha hali ya uharibifu wa faraja ya ndani kabisa ya nafsi ya mhusika. Wasanii wanachosema hapa ni kuwa chumba kama sehemu ya faragha na utulivu kinavamiwa hivyo hakuna tena sehemu salama ya kupumzika. Pia, kitanda ni ishara ya mapumziko na mahaba hivyo kinachafuliwa. Shati ni vazi la mwili, la utu linaguswa. Uvunjifu huu wa mipaka ya faragha unaonesha kiwango cha mateso ambacho kimeingia kwenye kiini cha utu wa mtu, kuharibu siyo tu mazingira yake ya nje, bali nafsi yake pia. Mohamed (1995) anaona kuwa mazingira ya nyumbani huweza kutumika kama uwanja wa kujieleza kwa kuwa ni mazingira ya kawaida kwa msanii na hadhira.

Bakize (2014) naye anaeleza kuwa jazanda za nyumbani hutoa uwezo wa kifani wa kugeuza vitu vya kawaida kuwa maumbo ya maana fiche. Kwa mfano, shati hapa linaweza kumaanisha mtu wa karibu sana na msanii, labda mpenzi wake, ambaye sasa "kunguni" ameweka doa au maumivu juu yake. Kitanda—kilichojaa mapenzi awali—sasa kimegeuka kuwa uwanja wa mateso. Kwa kutumia jazanda hizi, wasanii wanaufikisha ujumbe wao kwa kina bila kuwa wa moja kwa moja. Ni mbinu ya ficha-kwambua-funua, ambapo hadhira lazima itumie uelewa wa kijamii, kisaikolojia na kifasihi kufumbua maana. Hii ni njia ya kisanaa inayotaka ushirikiano wa hadhira katika kutengeneza maana .

Zaidi ya hayo, jazanda hizi zinaonesha hali ya kutojua pa kukimbilia. Mahali pa kukimbilia (nyumbani, chumbani) pamevamiwa na maumivu. Maana yake, maumivu ya kimapenzi yaliyovamiwa hapa hayatoi tena nafasi ya kutafuta faraja. Wasanii wamefanikiwa kuonesha kutoepukika kwa uchungu wa mapenzi na hata pa kujificha pakawa penye uchungu.

Katika muktadha huohuo wa matumizi ya jazanda, maneno ya mshororo usemao, "Kibatari utambi umetumbukia" nayo ni ya kipekee na yenye uzito mkubwa wa kimaudhui. Jazanda hii inaakisi ukosefu wa matumaini ya mwisho, hali ya kuzama gizani kiuhalisia na kiakili, na ni mfano halisi wa mawasiliano ya kihisia kwa kutumia taswira ya kawaida ya maisha ya watu wa chini. Kwa kuzingatia maana pana ya jazanda, hii inaweza kuchukuliwa kuwa ni jazanda jumuishi ya aina mbili: kwanza, ni *jazanda ya teknolojia ya zamani*, yaani kibatari kama chanzo cha mwanga kilichotumika kabla ya maendeleo ya nishati ya kisasa. Pili, ni *jazanda ya maisha ya watu wa vijijini au maskini*, ambao hadi leo bado wanategemea vyanzo vya mwanga kama vile kibatari kutokana na ukosefu wa nishati ya uhakika kama umeme.

Katika hali hiyo, kauli ya “kibatari utambi umetumbukia” ina maana pana zaidi ya kuzimika kwa mwanga na ni mfano wa mwisho kabisa wa matumaini yanapozimika hata kwa wale ambao tayari wanaishi gizani. Ujumbe huu unaeleweka kwa kina hasa kwa makundi ya watu waliokomaa kiumri, wanaoishi katika mazingira ya vijijini au watu wa daraja la chini ambao wanatambua kwa undani maana ya kibatari kama alama ya matumaini ya mwisho. Utambi wa kibatari unapotumbukia, mwanga huzimika, na hivyo hamna tena cha kuona, wala matumaini ya kuona tena hali inayolinganishwa na mapenzi yaliyofikia ukingoni bila njia ya kurejea.

Kwa kutumia jazanda hii, wasanii wamefanikiwa kuwasilisha hali ya *taabu ya kiroho, kihisia na kijamii* kwa namna inayogusa makundi maalumu kwa undani mkubwa. Kama asemavyo Buell (1995), mazingira na taswira zake za kila siku zinaweza kutumika kama daraja la kuelezea hali ya ndani ya binadamu na mabadiliko ya kijamii. Hii ni mbinu ya kifasihi yenye mashiko makubwa inayotoa fursa kwa msanii kushughulikia siyo tu hisia binafsi, bali pia changamoto za kitabaka, kimaendeleo na matumaini yaliyopotea kwa jamii pana.

4.4 Jazanda za Kibiashara

Katika kuendeleza uwasilishaji wa hisia na ujumbe wa mapenzi, wasanii wa wimbo *Kiza Kinene* wamechota taswira kutoka kwenye mandhari ya biashara, maeneo ambayo ni sehemu ya maisha ya kila siku ya mwanadamu. Biashara kama ilivyo nyumba, ni kiini cha maisha ya watu wengi, na kwa hivyo ni mazingira yanayotoa fursa pana kwa wasanii kuwasilisha ujumbe wao kwa kutumia lugha ya picha.

Katika ubeti wa kwanza wa wimbo huu, Nandy anaimba: "Nimezidisha chenji, (kibarua) kimeota nyasi..." Hili ni tamko lenye muktadha wa biashara. Katika lugha ya soko, "kuzidisha chenji" ni aina ya makosa katika miamala ya fedha, ambayo humletea mtu hasara. Kwa kutumia jazanda hii, msanii anaonesha kuwa katika mapenzi kuna makosa ambayo huweza kusababisha athari kubwa, yaani hasara ya kihisia au kimaisha. Hali hii inafafanuliwa zaidi na kusema "kimeota nyasi", akimaanisha kuwa kile kilichotarajiwa kuwa na thamani (mahaba, uhusiano) sasa kimeharibika au hakina faida tena. Muktadha huu unatoa taswira ya kupoteza kitu kilicho muhimu—sawa na mfanyabiashara anayepoteza mtaji wake.

Katika ubeti mwingine, tunaona maneno haya: "Sio fungu langu, nimekosea kuchagua". Hapa msanii anaonesha kuwa katika mapenzi, kama ilivyo sokoni au dukani, kuna mchakato wa kuchagua. Kuchagua kwa makosa kunaleta majuto. Katika biashara, "fungu" linaweza kumaanisha sehemu ya bidhaa au faida iliyotarajiwa, hivyo hapa anamaanisha kuwa alipata mtu ambaye hakuwa sahihi kwake, kama vile mteja au mfanyabiashara anavyopata bidhaa mbovu. Kama anavyosema Chum (1982), lugha ya picha inayochotwa kutoka katika maisha ya kila siku, ikiwemo biashara, hutoa fursa kwa msanii kujenga uhusiano wa karibu kati ya sanaa na jamii. Aidha, Senkoro (2011) anasisitiza kuwa matumizi ya mazingira yakiwemo ya kijamii kama biashara huongeza uhalisia wa kazi za fasihi na kuzifanya ziwe rahisi kueleweka kwa hadhira.

Katika ubeti wa kwanza tunakuta pia: "Nilipita dirishani nafasi kuigombania, kumbe basi limejaa na mlango upo wazi". Taswira hii ya "basi" inatumiwa kama biashara ya usafiri ambayo imejaa abiria. Msanii anaeleza kwamba alijitahidi kuingia katika uhusiano wa mapenzi kwa njia zisizo za kawaida (kupitia dirishani), lakini ikawa tayari nafasi zimejaa. Katika lugha ya biashara na maisha ya kawaida, hali kama hii huashiria kuchelewa au kukosa fursa. Kwa hivyo, kwa kutumia

mandhari ya biashara, wasanii wanaonesha kuwa mapenzi yanaweza kuwa na faida kubwa kwa mwanadamu, ustawi wa kihisia, kiakili na hata kijamii pia yanaweza kuwa chanzo cha maumivu, hasara na majuto kama hayataendeshwa kwa busara. Ulinganifu huu kati ya biashara na mapenzi unafanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira pana, hasa kutokana na ukweli kuwa biashara ni mandhari inayoeleweka kwa watu wa tabaka mbalimbali katika jamii.

4.5 Jazanda ya Imani za Kijadi

Katika uandishi wa kazi za kifasihi, jazanda za imani za jadi hutumika kwa njia ya kipekee kueleza hisia, mitazamo na hali ya kiroho ya wahusika au waimbaji. Wasanii Nandy na Sauti Sol wanatumia jazanda hizi kuakisi mguso wa ndani wa kisaikolojia na kiroho wa wahusika wao wa kimuziki, hususani katika kuonesha hali ya maumivu, mkanganyiko, na kukata tamaa katika mapenzi. Mfano wa jazanda kama “Haya ni marohani” inatoa taswira ya kiimani na kitamaduni iliyo na mizizi katika maisha ya Mwafrika. Matumizi ya neno "marohani" humaanisha kuhusika kwa nguvu zisizoonekana, kama vile mizimu au majini, katika matatizo ya kimapenzi au ya maisha kwa ujumla. Hili linapelekea msikilizaji au msomaji kuamini kwamba mateso anayopitia mzungumzaji si ya kawaida, bali yanaweza kuwa yamesababishwa na nguvu za kiroho au laana.

Kwa mujibu wa Temples (1959) na Abdallah (2018), imani za jadi ni msingi wa maisha ya Mwafrika na hufungamana na kila hatua ya maisha kama vile kuzaliwa, makuzi, ndoa, uzao, hadi kifo. Aidha, Okpewho (1992) anaeleza kuwa imani hizi zinapenyeza fasihi ya Kiafrika kwa namna ambayo huzipa kazi hizo muktadha wa kipekee wa kimaudhui na kisaikolojia. Vilevile, Wa Thiong’o (1986) anaongeza kuwa uhusiano kati ya mtu na jamii ya Kiafrika hauwezi kuachana na nguvu ya kiroho na tamaduni za kale.

Katika muktadha huu, matumizi ya jazanda kama “marohani” ni mfano wa kuwasilisha hali ya mtu anayesukumwa kuamini kuwa matatizo yake yanatokana na nguvu zisizoshikika. Ndossa (2023) anaeleza kuwa katika simulizi za kijadi kama zile za Ngoromiko kutoka Kware na Kwasadala, imani ya kuwapo kwa mizimu au viumbe wa kichawi kama mhusika Ngoromiko huonesha namna jamii huamini kuwa maisha ya mtu yanaweza kudhibitiwa au kuathiriwa na viumbe wa ajabu au nguvu za kimapokeo. Hili linaakisi jinsi msanii anavyotumia jazanda hizo kuelezea kushindwa kudhibiti mwelekeo wa mapenzi, hali ambayo kwa baadhi ya watu huweza

kueleweka kama "kupagawa" au "kurogwa". Kwa hivyo, jazanda za imani za jadi si tu mapambo ya lugha, bali ni zana thabiti za kimaana zinazosaidia kuwasilisha masuala mazito ya kihisia, kiimani, na kijamii katika kazi za kifasihi na sanaa za muziki.

5.0 Hitimisho

Kwa jumla, uchambuzi wa wimbo wa Nandy na Sauti Sol umeonesha kuwa jazanda ni mbinu ya kisanaa yenye uzito mkubwa katika kuwasilisha hisia fiche, dhana nzito, na hali halisi za kijamii, kiuchumi, kimazingira na kiutamaduni. Kupitia jazanda za viungo vya mwili, mazingira ya nyumbani, biashara, teknolojia ya kijijini na imani za jadi, wasanii hawa wameweza kufanikisha mawasiliano yenye mvuto wa kihisia na kina cha kimaudhui kwa hadhira yao. Jazanda hizi hutoa nafasi kwa wasanii kuelezea masuala magumu ya mapenzi, matumaini yaliyotoweka, au kukwama kwa uhusiano, kwa lugha ya picha na taswira ambazo hadhira inaweza kuzielewa kwa urahisi kutokana na ukaribu wake na maisha ya kila siku. Hili linaifanya sanaa ya muziki kuwa chombo cha kufundisha, kuonya, kuburudisha na kuibua tafakari za kina kuhusu maisha ya mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Kwa kuzingatia hoja na mawazo kutoka kwa wataalamu kama vile Buell (1995), Mohamed (1995), Bakize (2014), Temples (1959), Okpewho (1992), Wa Thiong'o (1986) na Ndossa (2023), makala hii imedhihirisha kuwa jazanda si tu mapambo ya lugha, bali ni njia ya kisanaa inayobeba historia, falsafa, imani na uhalisia wa Mwafrika. Ni njia ya msanii kusema mengi kwa maneno machache, kwa busara na kwa sauti ya undani inayogusa nafsi

Marejeleo

- Abdallah, S. (2018). Nafasi ya Fasihi ya Watoto ya Kidijiti katika Kukuza Fasihi Simulizi: Mifano kutoka Vibonzo Jongevu. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Bakize, L.H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Maccony Printing Press.
- Buell, L. (1995). *The Environmental Imagination: Thoreau, Nature Writing, and the Formation of American Culture*. Cambridge: Harvard University Press.
- Chum, H. (1982). *Desturi na Mila Zetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

- Lukács, G. (1962). *The Meaning of Contemporary Realism*. London: Merlin Press.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Mohamed, S.A. (1995). *Utangulizi wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Ndossa, S. A. (2023). Usawiri wa Mhusika Ngoromiko katika Masimulizi ya Kijadi: Mifano kutoka Vijiji vya Kware na Kwasadala. *Mwanga wa Lugha* Tol. 8(2), 95–103. Nairobi: Kenyatta University Press.
- Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds, Character, and Continuity*. Bloomington: Indiana University Press.
- Okwena, S. (2017). Mtindo wa Jazanda katika Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*. *Mulika* Na. 36, 1–15.
- Okwena, S. (2013). Matumizi ya Jazanda katika Tamthilia Tatu za Timothy Arege. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (hajachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Temples, P. (1959). *Bantu Philosophy*. Paris: Présence Africaine.
- Wa Thiong’o, N. (1986). *Decolonising the mind: The politics of language in African literature*. London: James Currey.
- Williams, R. (1977). *Marxism and literature*. Oxford: Oxford University Press.